**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI**

**TAARIFA KWA UMMA**

# MABADILIKO YA TAREHE ZA MITIHANI YA KATI YA KITAALUMA (MID SESSION PROFESSIONAL EXAMINATIONS) YA AGOSTI 2026

**Dodoma 29 Julai, 2026.**

**Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB)** inapenda kuwajulisha wadau wake kuhusu mabadiliko ya tarehe za kuendesha mitihani ya kitaaluma ya Kati kwa awamu ya pili (*2nd Mid Session Professional Examinations*) ya mwezi Agosti 2026. Mitihani hii sasa itafanyika Dodoma kuanzia tarehe **31/08/2026** hadi tarehe **04/09/2026** badala ya tarehe 24 – 28.08.2026 kama ilivyotangazwa awali. Waombaji wenye sifa na nia ya kufanya mitihani hii ya kitaaluma wanaelekezwa kufanya usajili wao kupitia **https://registration.psptb.go.tz** na kuendelea na maandalizi kupitia madarasa yao mahususi mafunzo.

## Waombaji wenye sifa ya kufanya mitihani ya kitaaluma ya agosti, 2026

(1) Wahitimu wote waliomaliza Vyuo vya Elimu ya Juu na Kati kwa ngazi za Shahada, Stashahada na Astashahada ya Ununuzi na Ugavi kwa kipindi cha kuanzia 2025 kurudi nyuma ambao hawakuwahi kufanya mitihani ya kitaaluma ya Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.

(2) Wafanyakazi wote wanaofanya kazi za Ununuzi na Ugavi katika sekta binafsi na umma pasipokuwa na cheti cha juu cha kitaaluma cha CPSP.

(3) Wahitimu wenye taaluma nyingine kuanzia ngazi za stashahada shahada au wenye sifa za kitaaluma kutoka Bodi/Mabaraza ya taaluma husika na yanayotambulika na Serikali ya Jahmhuri ya muungano wa Tanzania.

(4) Watahiniwa wa PSPTB waliomaliza mitihani ya kitaaluma ya Awali ngazi ya pili (Basic Stage II), mitihani ya kitaaluma ngazi ya Msingi (Foundation Stage I and II), Mitihani ya Kitaaluma ngazi ya kwanza, pili, tatu na nne (Professional Stages I, II, III and PIV) ndani ya miaka mitano kwa mujibu wa Mtaala wa Kitaaluma wa PSPTB.

(5) Watahiniwa wote wanaorudia baadhi ya masomo katika ngazi mbali mbali ndani ya miaka mitatu kwa mujibu wa matakwa ya Mtaala mpya.

**NB:**

(a) Watahiniwa wanaorudia mitihani zaidi ya ngazi moja wanaruhusiwa kuunganisha ngazi mbili zinazofuatana *(Two Consecutive Examination Levels)* kwa masomo kuanzia mawili hadi sita tu, na kwa kuzingatia ratiba ya mitihani hii Kati *(Mid session examinations)* ya PSPTB. Hivyo, wanaombaji wote **wanashauriwa** kuangalia ratiba ya mitihani husika kabla ya kuomba kufanya mitihani hiyo.

(b) Ada za mitihani hii zimewekwa kwenye tovuti ya PSPTB na dirisha la usajili sasa litafungwa **tarehe 16/08/2026** badala ya **07.08.2026.**

(c) Kwa maelezo au ufafanuzi zaidi tafadhali piga simu namba **0738441972** muda wa kazi au tuma barua pepe kupitia ***examinations@psptb.go.tz***

Digitally Signed By Alex Donald Mfungo
Wed Jul 29 14:45:12 EAT 2026

***PSPTB INAOMBA RADHI KWA USUMBUFU UTAKAOJITOKEZA***

***Imetolewa na:***

Alex Donald Mfungo
**DFA**